# Usawiri wa Familia ya Kisasa katika Fasihi ya Watoto Nchini Kenya

*Gatere Lucy Njeri, James Omboga Zaja na Rayya Timammy*
*Chuo Kikuu cha Nairobi*

**Ikisiri**

**Madhumuni ya makala haya ni kuhoji kwamba licha ya kuwepo kwa familia za aina mbalimbali na zilizo changamano nchini Kenya, watunzi wa hadithi za watoto wanaendelea kusawiri familia kiini ambazo kimsingi huwa na baba, mama na watoto, ilhali kihalisia wapo watoto wanaotokana na familia za mzazi mmoja, familia za malezi na wengine kutoka taasisi za malezi na hata familia ambapo walezi wa watoto ni babu na nyanya za watoto wanaolelewa. Kwa misingi hii kunaweza kutolewa hoja kwamba fasihi ya watoto ya kisasa nchini Kenya haiwasilishi upana, uchangamano na usasa wa kifamilia kwa sababu tathmini za hadithi nyingi za watoto zilizoko zinadhihirisha uhalisi wa usawiri wa familia wa aina moja na kwa hivyo kuibua fikra potovu kwamba watoto kama wahusika katika tungo mbalimbali za fasihi ya watoto wanatoka katika familia zinazowiana. Uhalisi huu wa chukulizi potovu za uwepo wa familia kiini katika hadithi za watoto unadhihirika katika vitabu viwili teule vya fasihi ya watoto - '*Mwepesi wa Kusahau*' na '*Likizo ya Mkosi*.' Usawiri wa familia katika vitabu hivi umekitwa katika uelewa banifu kwamba kimsingi, familia huendesha shughuli za kila siku kama familia kiini - yaani familia inayojumuisha baba, mama na watoto, familia isiyokuwa na mahusiano na familia pana. Makala haya yanapania kupendekeza kwamba utunzi wa hadithi za watoto unahitaji ujasiri wa kusawiri mifumo anuwai ya kifamilia inayojitokeza katika hadithi za watoto katika upana wake wa kiuchangamano ili kuwezesha kuakisika kwa mifumo na miundo yote ya kifamilia inayopatikana nchini Kenya. Hii itawezesha usomaji wa fasihi ya watoto shuleni kwenda hatua zaidi ya burudani na kutilia mkazo usomaji unaojenga ukuaji wa mitazamo chanya ya maisha miongoni mwa watoto wakiwa wangali wadogo kuhusiana na usawiri wa familia. Makuzi ya watoto na ufunzaji wa maadili ni mambo yawezekanayo sio katika misingi ya familia tu bali pia kupitia mafunzo ya fasihi ya watoto.**

**Maneno Muhimu**: Fasihi ya Watoto, Familia, Usawiri, Familia Kiini, Watoto

## Utangulizi

Kifungu cha 45 cha Katiba ya Kenya (2010) kinafafanua na kutoa maelekezi kwamba familia ni muungano wa kiasilia na wa kimsingi wa jamii na pia ni

kiungo msingi cha mpangilio wa kijamii na unaotambuliwa na kulindwa kisheria. Licha ya kwamba kuna ufafanuzi huu wa kikatiba na kisheria wa familia, uhalisi wa kifamilia na mifumo ya kifamilia nchini Kenya ni changamano sana. Hii ina maana kwamba katika utunzi wa fasihi ya watoto, kuna matarajio ya kuona ubainikaji wa uchangamano wa kifamilia unaoakisi uhalisi wa kimaisha. Kama anavyohoji Hunt (2002), kuna haja kuchunguza mambo yanayowasilishwa kwa watoto kupitia aina mbali mbali za fasihi ya watoto. Aidha, kuna haja kuchunguza mambo hayo anuwai yanavyosawiriwa na jinsi ambavyo usawiri huo una mafunzo kwa watoto. Usawiri wa familia katika hadithi za watoto na katika fasihi ya watoto kwa jumla ni mojawapo wa masuala muhimu yanayohitaji uchunguzi ili kubainisha fasihi ya Kiswahili inavyomwelewesha mtoto kuhusu dhana ya uhalisia wa kifamilia. Makala haya yanakusudia kuchunguza usawiri wa familia katika hadithi za watoto ili kuonyesha kama kuna upendeleo wa aina za familia zinazosawiriwa katika fasihi ya watoto ya Kiswahili. Hapana shaka, watoto ni kundi la jamii lililo na umuhimu mkubwa na linaloambatanishwa kwa karibu sana na familia kwa maana kwamba makuzi ya watoto, ufunzaji wa maadili na mbeko ni mambo yawezekanayo katika misingi ya familia. Hii ina maana kwamba kuna haja kuelewa na kuitambua mifumo ya kifamilia na jinsi inavyoathiri makuzi ya watoto.

**Umuhimu na Nafasi ya Fasihi ya Watoto katika Malezi**

Ngugi (2012) anafasili fasihi ya watoto kama fasihi iliyoandikwa kwa minajili ya kusomwa na watoto. Kwa upande wake, Bakize (2014) anaeleza kuwa fasihi ya watoto ni fasihi maalumu inayowahusu watoto kama walengwa na pia kama wahusika wa msingi katika fasihi hiyo. Fasili ya Bakize inaweza kuchukuliwa kuwa inaboresha na kwa kiasi fulani inaimarisha fasili ya Ngugi kwa kuwa Ngugi alirejelea fasihi iliyoandikwa tu ilhali Bakize anachukua mtazamo mpana sawia na alivyofanya Wamitila (2008), kwamba fasihi ya watoto yaweza kujumuisha fasihi iliyoandikwa au inayosimuliwa kwa mdomo. Fasihi ya watoto inajitokeza takribani katika tanzu zote za fasihi kama vile fasihi simulizi ya watoto na fasihi andishi. Kwa mujibu wa Miricho (2015), fasihi simulizi ya watoto inahusisha mashairi mepesi yanayoweza kuimbwa na kukaririwa na watoto, nyimbo za watoto, hadithi simulizi za watoto na tamthilia na maigizo mepesi ya watoto. Nayo fasihi andishi ya watoto inajumuisha hadithi za watoto, vitabu vya picha simulizi vya watoto, vitabu vya vibonzo vyenye wahusika watoto au vinavyokusudiwa watoto, mashairi mepesi yaliyoandikwa na tamthilia nyepesi. Miricho (2015) anaongezea kuwa ingawa wahusika wa fasihi ya watoto wanaweza kuwa wanyama, mazimwi na watu wazima kama vile wazazi na walimu wa watoto, wengi wao huwa watoto wenyewe ili kuweza sio tu kuvutia hadhira ya watoto lakini pia kufanya masuala yanayoshughulikiwa kuakisika kihalisi. Hali hii hufanya kazi ishawishi mtoto kuisoma kwa kuweza kujitambulisha na mhusika

mtoto mwenzake katika msuko wa hadithi nzima hasa iwapo mhusika yule ni shujaa na mwenye maadili. Miricho anaendelea kuhoji kwamba sera na mifumo ya elimu nchini Kenya imechangia pakubwa maendeleo ya fasihi ya watoto kiutunzi na kiusomaji nchini Kenya hasa kwa kuwa kupitia kwa somo la Kiswahili shuleni, watoto wengi wameweza kutangamana na kuvisoma vitabu vingi vya hadithi za watoto. Miricho, Sheila na Nabea (2019a) wanaeleza kuwa maendeleo ya fasihi ya watoto katika karne ya ishirini na moja yamepiga hatua kubwa kiasi cha kukiuka kanuni za fasihi hii kimaudhui kama zilivyowekwa na kuzoeleka katika kazi za miaka ya nyuma. Maoni haya yaliupa msukumo utafiti wa makala haya kwa kuchochea hamu ya kutaka kujua jinsi familia inavyosawiriwa katika hadithi za watoto.

Miricho na Mbuthia (2017) wanahoji kuwa usomaji wa fasihi ya watoto unaweza kuwaathiri watoto kama wasomaji kwa njia chanya au hasi kutegemea watoto wamesoma nini, walichokisoma kimesawiriwa kwa njia gani na kinasaidia kujenga uelewa na mitazamo gani ya kimaisha. Hivyo, ni muhimu kutilia maanani usawiri wa kifamilia unaojitokeza katika hadithi za watoto. Usawiri wa wahusika watoto unaweza kuathiri uamuzi watakaotoa watoto wanaosoma vitabu vya hadithi. Hii ni kwa sababu wanapokea ujumbe au maudhui yaliyoko hadithini kwa njia mbali mbali na wanaweza kukumbuka kwa urahisi yale waliyosoma hasa ikiwa ujumbe huo unaakisi ukweli fulani kuhusu maisha yao katika jamii. Hivyo basi, ipo haja ya kuhakiki vitabu vya hadithi za watoto ili kubaini ni nini kinachosomwa na watoto, kama watoto wasomi mambo faafu na yanayostahili kwa ajili ya kuwajenga kimaadili na kuwapa mielekeo inayofaa katika familia ili jamii iwe na vizazi bora vya siku za usoni.

Mbali na kukuza uwezo wa kiubunifu na kiutambuzi, fasihi ya watoto inaweza kuchangia ukuzaji wa tabia za watoto pamoja na ukuaji wao kijamii. Kwa sababu ya urahisi wa watoto kuathirika na kukubali yanayowasilishwa katika hadithi wanazosoma, hadithi hizo zinaweza kuchangia kuwakuza kuwa watu wazima wanaojali wenzao, watu walio na akili razini, werevu na wepesi wa kujenga urafiki na watu wengine. Fasihi ya watoto inaweza kuchangia kupiga vita tabia za ubinafsi, ubahili, uchoyo na tabia nyinginezo zinazokataliwa na jamii. Haya ni mambo ambayo sio tu yanajitokeza katika familia bali yanaathiri makuzi ya watoto katika miktadha ya kifamilia na hatimaye miktadha ya kijamii. Kukua kijamii kunaweza kutokana na watoto kusoma hadithi zinazowawezesha kuona jinsi watu wanavyohusiana katika miktadha ya kifamilia na hatimaye kijamii, hasa pale ambapo watoto wanawezeshwa kutambua hali tofauti za watoto wenzao, kwa mfano, katika misingi ya maumbile kama vile tofauti za jinsia, uwepo wa ulemavu, uwepo wa tofauti kati ya watoto katika misingi ya hali za utajiri na umasikini. Hadithi za watoto zina uwezo wa kukuza thamani ya kudumu kwa maana baadhi ya hadithi wanazosoma zinasalia akilini mwao katika maisha yao yote. Pamoja na haya, Miricho, Sheila na Nabea (2019b) wanahoji kwamba

fasihi ya watoto ina nafasi muhimu katika kumwezesha mtoto kuelewa masuala yanayomzingira. Hivyo, thamani ya fasihi ya watoto haishii na kusalia katika miktadha ya shule bali ina manufaa nje ya mipaka ya shule kwa kuwa ina ushawishi juu ya makuzi ya tabia. Kutokana na kauli hizi, sehemu ifuatayo itajaribu kuonyesha jinsi mambo haya, na hasa jinsi suala zima la usawiri wa familia linavyosawiriwa katika hadithi za watoto.

**Muhtasari wa *Mwepesi wa Kusahau***

*Mwepesi wa Kusahau* ni hadithi inayowahusu wahusika wakuu watoto Juma na Maria ambao ni wahusika binadamu katika hadithi ya hii. Juma na Maria ni watoto wa Hamisi Akida ambaye ni tabibu wa mifugo wilayani Kericho na Lilian Mokeira, muuguzi mkuu katika hospitali ya wilaya hiyo ya Kericho. Watoto hawa walifanana sana katika maumbile yao japo walitofautiana katika hulka zao. Wazazi wa watoto hawa wanawapenda sana wanao na wanawashughulikia kwa dhati kwa kuhakikisha kwamba wanawapa malezi bora na elimu kwani wanaamini ya kwamba elimu ndiyo ufunguo wa maisha. Juma na Maria ni wanafunzi wa darasa la nne katika shule ya msingi ya Jengahekima. Tofauti za tabia na hulka zao zinadhihirika katika maisha yao ya shuleni. Maria ni mwanafunzi nadhifu na mwenye bidii masomoni, ni mwadilifu anayeweka makini katika kila analolitenda shuleni na ana kumbukuzi nzuri juu ya masomo yake. Nidhamu hii inamfanya kupendwa na kuthaminiwa na walimu na wazazi wake. Kwa upande wake, Juma si mtoto mwadilifu na kwa sababu hii anakumbana na matatizo mengi shuleni na nyumbani. Hatilii masomo maanani na ana tabia ya kusahau mambo haraka. Juma ni mwanafunzi mchafu kwa njia nyingi akilinganishwa na dada yake Maria, hafanyi kazi zake za shule kwa wakati, hana unadhifu anapozifanya na anapenda sana kulala kupita kiasi. Juma ni tofauti sana na Maria ambaye aliiga mambo mengi mazuri kutoka kwa wazazi wake, walimu na wanafunzi wenzake walio na tabia nzuri. Baadhi ya tabia nyingine nzuri aliziiga kutoka kwa babake, mathalani tabia ya kuwa na shajara kwa ajili ya kuandika alichoagizwa na kuweka kumbukumbu. Maria ana mazoea ya kuamka mapema na kujitayarisha kwa ajili ya kwenda shuleni. Mama yao alihakikisha kila wakati amewashughulikia wanawe asubuhi na mapema kwa kuwatayarishia kiamshakinywa na mambo sawia na hayo.

Utovu wa nidhamu wa Juma unamfanya kukosana na wazazi wake, ndugu yake, walimu wake na hata wanafunzi wenzake. Una uzohali wa kujitayarisha kwenda shuleni, anachelewa kufanya mambo mengi kwa wakati, usafi wake haupendezi, ni msahulifu wa mambo mengi kama vile anapoziweka kalamu zake, vitabu na mambo mengi ya kibinafsi. Juma ana tabia ya kuchelewa shuleni ambayo mara kwa mara inamfanya kuadhibiwa mbele ya wanafunzi wote. Kwa jumla japo Juma na Maria ni ndugu, walitofautiana kabisa kitabia, Maria alikuwa nadhifu wa kutamanika ilhali Juma alikuwa mchafu kuchukiza. Lakini kwa

sababu za kuhusika kwa walimu na wazazi wake, Juma akaamua kuzika tabia zake mbaya na kuiga mfano mwema kama wa dada yake Maria. Maudhui ya kimsingi yanayojitokeza katika hadithi hii ni yale ya maadili yanayosisitiza tabia nzuri, ushirikiano, upendo, bidii na uwajibikaji—uwajibikaji wa watoto na wazazi katika majukumu yao. Maudhui mengine ni elimu ya watoto, mambo yanayotoa mafunzo yatakayowafaa watoto kama wasomaji, lakini lililo muhimu zaidi ni kwamba yanawezeshwa kwa sababu yamesawiriwa katika misingi ya familia adilifu na familia kiini.

**Muhtasari wa *Likizo ya Mkosi***

*Likizo ya Mkosi* ni hadithi inayowahusu wahusika wakuu wawili, Otambo na Kerubo na wazazi wao na jamaa zao wa karibu. Otambo na Kerubo ni watoto ndugu wa toka nitoke, watoto wa Dkt. Stephen Ogato mtafiti katika kampuni ya majani chai ya Bubondi wilaya ya Chorike. Kerubo na Otambo walisoma katika shule ya msingi ya Majimazuri, katika darasa la sita na tano mtawalia. Ni watoto waliowatambua na walitamani sana kwenda kuwasalimia babu na nyanya yao mashambani shule zikifungwa muhula wa tatu. Baba yao aliwaahidi kuwapeleka mashambani mwishoni mwa muhula lakini kwa masharti kwamba wafanye bidii katika masomo yao ndio ndoto yao ya kwenda mashambani itimie. Katika mitahani ya mwisho wa muhula huo waliibuka washindi katika madarasa yao na wakatuzwa zawadi. Wakati wa likizo baba yao alitimiza ahadi yake kwani aliwapeleka mashambani kwenda kuwajulia hali babu na nyanya yao. Baada ya kuwafikisha nyumbani mashambani, Dkt. Ogato alifunga safari ya kwenda Tanzania. Walipokuwa likizoni kwa babu na nyanya yao, zilikuja taarifa za baba yao kuhusika katika ajali barabarani akitoka Arusha kuja Nairobi na kwamba alikuwa amelazwa hospitalini Nairobi, jambo lililokatisha likizo yao kwa ghafla. Watoto hawa na babu na nyanya yao walisafiri kwenda kumwona majeruhi ambapo waliungana na mama yao. Siku chache baadaye Dkt. Ogato alipata nafuu na kuruhusiwa kuondoka hospitali. Kerubo aliiona likizo yao kama likizo ya mkosi na kwa pamoja walimshukuru Mungu kwa kumnusuru na kumlinda baba yao. Kimaudhui, *Likizo ya Mkosi* ni hadithi iliyo na maudhui mengi ya kimaadili yanayoangazia maisha ya kifamilia, mahusiano ya kifamilia, ushirikiano, upendo na uwajibikaji. Maudhui mengine yanayojitokeza ni elimu ya watoto na uchumi hasa kuhusiana na shughuli za Dkt. Ogato kuhusu majani chai.

**Aina ya familia inayosawiriwa katika hadithi zilizoteuliwa**

Katika hadithi ya *Mwepesi wa Kusahau,* familia iliyojitokeza ni familia kiini (*nucleus family*). Hii ni familia inayojumuisha wazazi wawili—baba na mama na watoto wao. Aina hii ya familia inadhihirika vyema kutokana na maelezo yafuatayo; “Wazazi wa Juma na Maria walifurahia sana walipobarikiwa na kupata watoto mapacha. Baba yao Hamisi Akida, alikuwa tabibu wa mifugo

wilayani Kericho. Mama yao Lilian Mokeira alikuwa muuguzi mkuu katika hospitali ya wilaya hiyo. Wote waliwapenda sana wanao. Walijitahidi kwa hali na mali kuwapa malezi bora na elimu. Waliamini kuwa elimu ndiyo ufunguo wa maisha (uk.7). Maelezo yanayotolewa kuhusu wasifu wa familia hii yanadhihirisha kuwa hii ni familia kiini kwa kuwa Juma na Maria wanalelewa na wazazi wawili, Hamisi Akida baba yao na mama yao Lilian Mokeira. Mwandishi anadhihirisha ya kwamba katika familia hii wazazi ni wafanyikazi walioajiriwa na kwa hivyo wana kipato. Ni familia ya kisasa ambayo imepuuza misingi ya ukabila ikizingatiwa kwamba wanandoa hawa wametoka katika jamii tofauti na kuunda familia yao isiyotawaliwa na misingi ya kikabila. Familia hii ni ithibati ya aina mpya ya familia za kisasa zinazopatikana nchini Kenya. Ni familia ambayo ina baba, mama na watoto. Wazazi hawa halisi wanawalea wana wao vilivyo kadri ya uwezo wao wa kihali na kifedha. Ni familia iliyo na mahusiano ya kimji na kishamba ikizingatiwa kwamba mama ni muuguzi katika hospitali ya wilaya na baba ni daktari wa mifugo katika wilaya hiyo.

Katika familia hii, ambayo ni familia kiini, watoto wanaonekana kupendana na kuhurumiana. Kwa mfano, Maria anavyomhurumia ndugu yake na kumsaidia kurekebisha tabia yake. Hatimaye, Juma licha ya kuwa na matatizo mengi kama vile kusahau mambo kwa wepesi, kuwa mchafu na mzembe aliweza kubadilika na kuiga mfano mwema wa Maria. Juma alianza kuiga mambo yote mazuri ya Maria kama vile kukumbuka mambo na kuwa safi na mwenye bidii. Pamoja na kwamba hadithi hii imewezesha kubainika kwa maudhui ya kimaadili, ni hadithi ambayo inasimuliwa na kusawiri familia isiyokuwa na mahusiano na jamii pana. Ni familia isiyotangamanishwa na majirani, haina msambao wa kimahusiano na jamii pana, watoto hawana marafiki, hawatangamani na watoto wengine kiasi kwamba inakuwa vigumu kuelewa Juma alitoa wapi tabia hizi za uzohali na uzembe. Katika miktadha ya kifamilia inaweza kudaiwa kwamba tabia ni matokeo ya ushawishi wa mifumo pana ya kimahusiano.

Katika hadithi ya *Likizo ya Mkosi*, familia inayojitokeza ni familia kiini. Familia hii inajumuisha watoto na wazazi wao kama inavyoelezewa katika (uk. 1) tunapoelezewa kuhusu baba yao kuwa aliitwa Dkt. Stephen Ogato na alikuwa mtafiti katika kapuni ya majani chai ya Bubondi. Mama yao hajatajwa kwa jina lakini anatambulika vyema katika mazungumzo yake na watoto wake katika (uk.5) baada ya Otambo na Kerubo kufunga shule na kurudi nyumbani kwa likizo. Familia hii kiini inajihusisha na kushirikiana na familia pana inayohusisha babu na nyanya na watoto wa familia kiini, japo kwa njia kadha wa kadha haina majirani au watu wengine wanaohusiana nao. Familia kiini inaishi mjini lakini mara kwa mara hutembea mashambani ambapo wanajiunga na babu na nyanya na kuwa familia pana. Kama inavyoelezewa katika (uk. 22) kuwa, walipofika kwa babu na nyanya walikaribishwa kwa furaha. Familia kiini inaonekana kuwa na maisha ya kisasa ambapo watoto wanashughulika na masomo yao shuleni wakati

baba yao anafanya kazi ya kuajiriwa katika miji mbalimbali mbali na nyumbani. Familia hii kiini na familia pana zinaonekana kuwa na uhusiano wa karibu sana huku kila mmoja akimjali mwenzake kama inavyoonekana baba yake Kerubo anapohusika katika ajali ya barabara. Wanafamilia kutoka familia kiini na familia pana walikutana hospitalini Nairobi kumwona. Kwa muhtasari, aina za familia zinazosawiriwa katika vitabu hivi viwili ni familia kiini. Kila familia kwenye vitabu hivi ina baba, mama na watoto wao. Hii imeonekana kuwa familia inayopendelewa zaidi na waandishi wa fasihi ya watoto na ambayo watoto wengi wasomaji wa hadithi wanaweza kujihusisha nayo.

**Usawiri wa familia kama taasisi katika vitabu vilivyoteuliwa**

Familia katika *Mwepesi wa Kusahau* imesawiriwa kama familia iliyoipa elimu kipaumbele. Awali wazazi wa familia hii wamesawiriwa kuwa ni watu waliosoma na ni wana taaluma ambao wanafanya kazi ya ajira, wana kipato, wametoka katika jamii tofauti, hawakufungika katika ada ama itikadi za jamii moja na ni wazazi wa kisasa. Uthamini wao wa masomo unaonekana wazi wakati Juma na Maria walipohitimu umri wa kwenda shule. Katika (uk. 8) tunaelezewa kuwa wazazi wao waliwatimizia mahitaji ya shule kwa kuwanunulia sare, vitabu vya kusoma, madaftari na kalamu pamoja na mikoba ya kubebea vitabu vyao. Wazazi wao walikuwa kielelezo kizuri kuhusu elimu. Baba yao aliyeitwa Hamisi Akida alikuwa amesoma na kuwa tabibu wa mifugo. Mama yao naye alikuwa amesoma hadi akawa muuguzi mkuu katika hospitali ya wilaya hiyo.

Usawiri mwingine unaojitokeza katika familia ya *Mwepesi wa Kusahau* ni kuwa mtoto mvulana amelimbikiziwa sifa hasi ilhali msichana anasawiriwa kwa njia chanya. Juma anachukuliwa kuwa mtovu wa nidhamu ilhali Maria anasawiriwa kama mwenye kuwajibika. Kwa mfano, katika (uk. 9) tunaelezewa kuhusu tabia ya Juma ikilinganishwa na ya Maria kuwa Juma hakutilia masomo maanani ilhali Maria alikuwa akifanya vizuri shuleni. Juma pia alikuwa na tabia ya kusahau haraka mambo mbalimbali aliyoambiwa afanye huku Maria akiwa anakumbuka mambo kwa wepesi. Kwa upande mwingine, familia ya *Mwepesi wa Kusahu* inasawiriwa kama iliyo na ushirikiano na mshikamano mzuri baina ya wazazi na watoto na watoto kwa watoto. Mama anaonekana kuwaelewa watoto wake vizuri na kuwasaidia ifaavyo bila kugombana nao. Ushirikiano unajitokeza kwenye familia kati ya watoto na wazazi wao. Watoto walikuwa wakiwasaidia wazazi wao wakati wa likizo kwa kazi mbalimbali. Mifano ya kazi walizowasaidia wazazi wao kuzitekeleza zinaelezewa katika (uk. 12-13). Juma na Maria wakiwa nyumbani wakati shule zimefungwa waliwasaidia wazazi katika kazi ya kuwalisha kuku, kuwapa maji ya kunywa pamoja na kukusanya mayai kutoka kwenye viota na kuyatia vikapuni ili yakauzwe.

Familia ya *Mwepesi wa Kusahu* inasawiriwa kwa njia mbalimbali kutegemea sifa za wahusika na nafasi zao katika shughuli za kifamilia, lakini kimsingi

inasawiriwa kama familia kielelezo. Katika familia hii kila jambo linalotarajiwa katika familia lipo linapostahili kuwa, majukumu yanayotarajiwa kutekelezwa yanatekelezwa, kipato kinachotakikana kuiendeleza familia kipo, mazingira yanayochangia makuzi mazuri ya watoto yapo, alimradi kila jambo lipo mahali pake. Kimsingi baba alitajwa tu na hakuonekana tena katika familia akitekeleza majukumu muhimu katika kuendeleza familia. Mama ndiye anayeonekana kushughulikia mahitaji ya watoto na maendeleo ya familia tangu mwanzo hadi mwisho. Mathalani, mama ndiye anayewaandaa watoto kabla ya kwenda shuleni (uk. 19), ndiye ambaye watoto wanatafuta ushauri kwake wanapohitaji msaada (uk. 20) na ndiye anayechukua majukumu ya kumsaidia Juma ili aweze kuboresha mienendo yake na kutilia maanani masomo (uk. 30). Pamoja na ukamilifu huu wa kifamilia kuna masuala ibuka katika usawiri wa familia hii. Juma, mtoto wa kiume anasawiriwa kwa njia kinzani kwamba japo ni mwepesi wa kusahau anachangia katika kazi za kifamilia wakati wa likizo. Suala lingine ambalo linaweza kuhusishwa na usawiri wa Juma linaweza kuhusishwa na utelekezwaji wa watoto wa kiume ikizingatiwa kwamba hadithi hii imetungwa katika kipindi ambapo masuala ya utetezi wa haki za mtoto msichana yaliwekwa mbele zaidi kuliko mahitaji ya mtoto mvulana. Suala hili hata hivyo, mtunzi hakulikuza kwa ukamilifu. Suala ambalo mtunzi ameelekea kukuza kwa ukamilifu ni usawiri chanya wa mtoto wa kike kama mtoto safi, mwenye kuwajibika, mwenywe bidii na mfano mwema kwa jumla wa kuigwa na watoto wengine.

Katika hadithi *Likizo ya Mkosi*, familia iliyojitokeza ni familia iliyo na wazazi wote wawili, yaani baba na mama ambao walishirikiana katika majukumu yote ya kuwalea wana wao. Kwa mfano, katika kuwapa chakula, mavazi, afya bora na hata elimu. Pia familia yote ilipenda kutangamana na jamaa wao wengine wote ndiposa wazazi waliwapeleka wana wao kwenda kuwasalimia nyanya na babu mashambani wakiwa wamewabebea zawadi (uk. 26). Jambo hili la kuwabebea zawadi linaonyesha maadili ya upendo katika familia. Nyanya na babu walishukuru huku wakisifu zawadi walizopelekewa. Familia hii inasawiriwa kama iliyopenda elimu ya watoto wao. Jambo hili ladhihirika katika ukurasa wa 1 ambapo baba anawahimiza kutia bidii masomoni kwa kuwaahidi kuwatembeza kwa nyanya na babu ikiwa watafanya vizuri masomoni.

Familia hii pia inasawiriwa kama yenye watoto walio na bidii. Bidii ni maadili muhimu katika makuzi ya watoto. Walijua kibali chao cha kwenda mashambani kuwasalimia nyanya na babu kitatokana na kufanya vyema kwenye mtihani wao wa mwisho wa muhula. Kwa jumla, inabainika kuwa katika hadithi ya *Mwepesi wa Kusahau* ambapo baba ametajwa katika (uk. 1) pekee kuelezea kuwa alikuwa tabibu wa mifugo wilayani Kericho, familia ilisawiriwa kama ambayo inashughulikiwa na mama zaidi ya baba hasa kuhusu malezi ya watoto na shughuli nyingine za maisha ya kila siku. Katika hadithi ya pili, *Likizo ya Mkosi*, hali hii inaendelea kubadilika ambapo baba katika familia anasawiriwa

kama anayeshughulikia majukumu yake vilivyo. Baba anaonekana akishirikiana na mama katika maisha ya kila siku katika malezi ya watoto wake. Usawiri mwingine muhimu wa kifamilia ni kuhusu mitazamo ya kielimu. Katika hadithi zote mbili watoto katika familia wanahudhuria shule na suala la kufanya bidii masomoni ili waweze kufanikiwa linatiliwa maanani. Aidha, familia hii inasawiriwa kama yenye maadili ya umoja na ushirikiano. Ushirikiano unajitokeza baina ya wazazi wenyewe, kati ya wazazi na wana wao na baina ya watoto wenyewe katika familia. Katika hadithi ya *Likizo ya Mkosi* mama anaamka mapema kuwatayarishia wanawe kiamshakinywa huku baba naye akikubali kuwapeleka watoto mashambani. Watoto nao walikubali kujitayarisha tayari kuondoka. Mfano mwingine wa ushirikiano unapatikana katika (uk. 50) wakati ambapo baba alipata ajali na kulazwa katika hospitali ya Nairobi. Nyanya, babu, wajukuu na mama wote walishirikiana kwenda kumjulia hali baba katika hospitali. Hii inaonyesha familia kiini na familia pana kwa jumla zilishirikiana kuendeleza maadili ya familia kama taasisi.

**Hitimisho**

Katika hadithi zilizochunguzwa kwa utafiti wa makala haya, familia zilizojitokeza ni familia kiini. Mjadala tulioundeleza hapa umebainisha kuwa watunzi wa hadithi za watoto wanaendelea kusawiri familia kiini katika kazi zao licha ya kuwepo kwa uanuwai wa familia kama vile familia za mzazi mmoja, familia za malezi na hata familia ambapo walezi wa watoto ni babu na nyanya za watoto wanaolelewa. Hivyo, fasihi ya watoto ya kisasa nchini Kenya inaonekana kutowasilisha upana, uchangamano na usasa wa kifamilia na kwa hivyo kuibua fikra potovu kwamba watoto kama wahusika wanatoka katika familia za aina moja. Kauli ya kimsingi inayojitokeza ni kwamba usomaji wa fasihi ya watoto shuleni unahitaji kuwa na uhalisia mpana unaokiuka mipaka ya burudani, na badala yake kutilia mkazo uzingatiaji wa masuala mengine mapana yanayojumuisha ujenzi wa mitazamo chanya miongoni mwa watoto. Watunzi wa hadithi za watoto wanahitaji kutambua kuwa watoto ni kundi la jamii lililo na umuhimu mkubwa na linaloambatanishwa kwa karibu sana na familia. Kuna haja kuhakikisha kuwa katika kukuza mafunzo katika hadithi za watoto yanayohusiana na maadili ya kifamilia, kuna haja pia ya kuwafahamisha watoto masuala mengine yanayoathiri maisha yao ya baadaye. Ni muhimu fasihi ya watoto ilenge kuwapa watoto mafunzo haya kutokana na usomaji unaolenga kimakusudi haja kuelewa na kuitambua mifumo ya kifamilia na jinsi inavyoathiri makuzi yao.

**Marejeleo**


Bakize, L. H. (2014). *Utangulizi wa Fasihi ya Watoto*. Dar es Salaam: Moccony Printing Press.

Hunt, P. (2002). *Understanding children's literature*. Taylor & Francis e-library.

Matundura, B. (2005). *Mwepesi wa Kusahau*. Nairobi: Phoenix.

Matundura, B. (2014). *Likizo ya Mkosi*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Miricho, E. M. (2015). Usawiri wa Watoto katika Hadithi za "Mwepesi wa Kusahau" na "Likizo ya Mkosi". Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi.

Miricho, M. na Mbuthia, E. M. (2017). The Impact of the Depiction of Children in Selected Swahili Children Stories katika *The International Journal of Contemporary Applied Sciences*. Vol 4, No. 1, January, 2017 (ISSN: 2308- 1365).

Miricho, M., Sheila P. Wandera-Simwa na Nabea Wendo (2019a). "Ukiushi wa "Kanoni" ya Maudhui katika Fasihi ya Watoto ya Kiswahili" katika https://coretrain.org/wp-content/uploads/2019/07/CORETRAIN-JOURNAL-APRIL-2019-VOL-ONLINE-ISSUE.pdf ukurasa 77 - 85.

Miricho, M., Sheila P. Wandera-Simwa na Nabea Wendo (2019b). "Fasihi ya Watoto ya Kiswahili na Mshikamano wa Kitaifa" katika *Mwanga wa Lugha– Makala Teule ya Kongamano la CHAKITA 2018* (ISSN: 2412-6993), Moi University Press.

Ngugi, P. M. Y. (2012). "Tafsiri katika Fasihi ya Watoto: Mbinu na Mikakati." katika: S. Omari na G. Mrikaria (wh) *Mulika*. TATAKI, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na. 31. 2012 12 - 26 ISBN 0856-0129.

Wamitila, K. W. (2008). *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchangunuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide-muwa Publishers.